جمعية خدمة المحتوى
الإسلامي باللغات

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com



# Adabu za safari na hukumu zake

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

شركاء التنفيذ :

دار الإسلام
بيان الإسلام
رواد التراجم
المحتوى الإسلامي

يتاح طباعة هذا الإصدار ونشره بأي وسيلة مع
الالتزام بالإشارة إلى المصدر وعدم التغيير في النص

Tel : +966 50 244 7000
info@islamiccontent.org
Riyadh 13245-2836
www.islamiccontent.org

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, na rehema na amani ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad, na aali zake na Maswahaba zake wote.

**Ama baada ya hayo:**

**Hii ni makala fupi kuhusu adabu za safari na hukumu zake. Tumepupia ndani yake kuweka wazi mambo ambayo aghalabu anayahitajia msafiri.**

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aifanye iwe kwa ajili ya uso wake mtukufu, na anufaishe kwayo Waislamu wote.

**Jumuiya ya Masomo mbalimbali ya Kiislamu katika lugha mbalimbali**

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

# Adabu za safari na hukumu zake



# Kwanza: Adabu za safari

Mwenye kusafiri kwenda Hija au safari nyingine ya kiibada anafaa kuzingatia yafuatayo:

**Amuombe Mwenyezi Mungu Mtukufu amchagulie muda sahihi wa safari, kipando, rafiki wa kuendana naye, na muelekeo wa njia ikiwa njia zitakuwa nyingi. Na awatake ushauri kuhusu safari hiyo watu wenye uzoefu na wale walio wema.**

- Ama Hija na Umra, ibada hizo ni za heri na hakuna shaka katika hilo.
- Na namna ya kumuomba Mwenyezi Mungu amchagulie jambo ni: Aswali rakaa mbili kisha aombe dua iliyopokelewa kutoka kwa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.



## Ni wajibu kwa mwenye kufanya ibada ya Hija na Umra akusudie katika Hija yake na Umra yake uso wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kujiweka karibu naye,

na ajihadhari na kukusudia starehe za kidunia au , kujifaharisha au kupata umaarufu au kujionyesha au kutaka kusikiwa; kwani kufanya hivyo kunasababisha kuharibika kwa matendo na kutokubaliwa kwake.

## Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

Sema:"Mimi ni mwanadamu tu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Kwa hivyo, mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi, basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi".

## Na katika Hadithi takatifu:

**"Mimi ndiye niliyejitosheleza zaidi kuhitaji mshirika. Atakayefanya jambo lolote akamshirikisha pamoja nami mwingine, nitamuacha yeye na shirki yake (au na mshirika wake)"**



ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

## Ni wajibu kwa mwenye kufanya ibada ya Hija na Umra kujifunza hukumu za Umra na Hija, na kujifunza hukumu za safari kabla ya kuanza safari,

ili asijekuwacha jambo la wajibu au akafanya jambo la haramu. Amesema Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake -:

“Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemtakia heri, humpa ufahamu wa dini”

## Ni wajibu kwa mwenye kukusudia kufanya Hija au Umra achaguwe mali halali kwa ajili ya ibada yake ya Hija na Umra;

kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mzuri na hakubali isipokuwa kilicho kizuri; na kwa sababu mali haramu husababisha kutojibiwa maombi.

## Kutubia madhambi yote na maasi,

na ikiwa aliwadhulumu watu, atarudisha alichokidhulumu na kuwataka wamwachilie. Ni sawa dhuluma hiyo iwe ni kuhusiana na heshima, mali au haki nyingine.

## Inapendekezwa kwa msafiri aandike wasia wake,

na kuandika anachodai na anachodaiwa. Amesema Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu, ziwe juu yake:

“Sio haki ya mtu Muislamu mwenye jambo analotaka kulitolea wasia alale siku mbili, isipokuwa ahakikishe kwamba anao wasia wake pamoja naye tayari umeshaandikwa”

Na auwekee wasia huo mashahidi, na alipe madeni anayodaiwa, na arudishe amana kwa wenyewe au awatake idhini ziendelee kubakia kwake.

**Inapendekezwa kwa msafiri ajitahidi kuchaguwa rafiki mwema na apupie kwamba yule amchaguaye ni miongoni mwa wanafunzi wenye kujifunza elimu ya sheria;**

kwani kufanya hivyo ni sababu ya kufanikiwa na kuepuka kuingia kwenye makosa katika safari yake na katika ibada yake ya Hija na Umra. Haya ni kwa ushahidi wa maneno ya Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake ):

> “Mtu huwa katika mwenendo wa mwendani wake. Basi na aangalie mmoja wenu ni nani anayemfanya kuwa mwendani wake”

Na kwa maneno yake Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

> “Usifuatane katika safari zako isipokuwa na Muumini na asile chakula chako isipokuwa mchamungu”






## Inapendekezwa kwa msafiri kuwaaga watu wake, jamaa zake wa karibu, majirani zake na marafiki zake.

Amesema Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

«Yeyote anayetaka kusafiri, basi na awaambie wale anaowaacha: Astaudiukumullahu alladhiy laa tadhwiiu wadaa'iuhu (Ninawaacha katika amana ya Mwenyezi Mungu ambaye amana zake hazipotei»

Na alikua Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - akiwaaga maswahaba zake anapotaka mmoja wao kusafiri. Alikuwa akisema:

«Astaudiullaaha diinaka, wa amaanataka, wa khawaatiima a'malika (Ninamkabidhi Mwenyezi Mungu dini yako, na amana yako na mwisho wa matendo yako)»

Na alikuwa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - akimwambia msafiri mwenye kumtaka Mtume ampe wasia :

«Zawwadaka llaahut taqwa, waghafara dhambaka, wayassara lakal khaira haithu ma kunta (Mwenyezi Mungu akupe uchamungu, na akusamehe dhambi zako na aifanye kheri kuwa nyepesi kwako mahala popote utakapokuwa)»

Na alikuja mtu mmoja kwa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - akitaka kusafiri na akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nipe wasia.' Akasema:

**«Ninakuusia kumcha Mwenyezi Mungu, na kuleta Takbiira kila unapofika sehemu ya muinuko»**

Alipoondoka, Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, akamuombea kwa kusema:

**«Ewe Mwenyezi Mungu, mkunjie ardhi na umfanyie safari yake kuwa nyepesi»**

## Asiandamane na kengele wala gitaa wala mbwa katika safari,

kwa ushahidi wa Hadithi ya Abuu Huraira - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kwamba Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alisema:

**«Malaika hawaandamani na msafara ambao ndani yao kuna mbwa au kengele»**



## Na akitaka kusafiri na mmoja kati ya wake zake, ikiwa ni mwenye mke zaidi ya mmoja ,atawapigia kura ,na mke yeyote atakeyeangukiwa na kura ndiye atakaye safiri naye,

kwa ushahidi wa hadithi ya Aisha - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kwamba alisema:

> Alikuwa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - akitaka kusafiri, anapiga kura kati ya wake zake, na yeyote ambaye utatoka mshale wenye jina lake, basi huyo ndiye aliyekuwa akisafiri pamoja naye

## Inapendekezwa kwa msafiri asafiri siku ya Alhamisi mwanzo wa mchana ikiwa ni wepesi kwake;

kwa sababu Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake -alikuwa akifanya hivyo. Amesema Kaab ibnu Maalik - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

> Ni mara chache sana alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu yake, akitoka kwenda safarini isipokuwa angetoka siku ya Alhamisi

## Inapendekezwa kwa msafiri aombe dua ya kutoka nyumbani wakati wa kusafiri na wakati mwingine usiokuwa wa safari. Atasema wakati wa kutoka:

**Bismillahi. Tawakkaltu ala llahi walaa haula walaa quwwata illa billah. Allahumma inniy auudhubika an- adhwilla au udhwalla, au azilla au uzalla, au adh-lima au udh-lama, au aj-hala au yuj-hala alaiyya (Kwa jina la Mwenyezi Mungu. (Ninatoka) nimetegemea kwa Mwenyezi Mungu na hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Mwenyezi Mungu. Ewe Mola wangu wa haki, ninajilinda kwako kutokana na kupotea au kupotezwa, au kuteleza au kutelezeshwa, au kudhulumu au kudhulumiwa, au kuwa mjinga au kufanywa mjinga)**

## Inapendekezwa kwa msafiri aombe dua ya safari;

au gari lake, au ndege, au kipando kingine chochote. Hivyo atasema:

**(Allahu Akbar, Allahu Akbar, sub-hanalladhii sakhara lana haadha, wamaakunna lahuu muqriniina, wainna ilaa rabbina lamunqalibuuna. Allahumma inna nas-aluka fii safarina haadha al-birra wat-taqwaa, waminal amali maa tar-dhwaa. Allahumma hawwin 'alaina safarana haadha, wat-wi 'anna bu'udahu. Allahumma antas-swaahibu fis-safar, wal-khaliifatu fil-ahli. Allahumma inniy a'udhubika min wa'athaais-safar, waka-aabatil man-dhwar, wasuu-il munqalabi fil maali wal-ahli (Mwenyezi Mungu ni mkubwa, Mwenyezi Mungu ni mkubwa, Mweyezi Mungu ni mkubwa. Utakasifu ni wa Mwenyezi Mungu ambaye ametutiishia haya na tusengeliweza kuyadhibiti, na kwa hakika kwa Mola wetu Mlezi bila shaka tutarejea. Ewe Mola wetu wa haki, tunakuomba katika safari yetu hii wema na uchamungu, na tufanye matendo unayoyaridhia. Ewe Mola wetu wa haki, tufanyie wepesi safari yetu hii, na ufupishe umbali wake. Ewe Mola wetu wa haki, hakika Wewe ndiye mwenza katika safari hii, na mchungaji wa familia yangu. Ewe Mola wetu wa haki, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ugumu wa safari, na ubaya wa mtizamo na kurudi kubaya kwenye mali na familia)**[123]

---

(1) Neno "Al-munqalab" ni kurudi. Maana hii inapatikana katika kitabu kiitwacho Al-ifswaahu 'an Ma'aani As-swihaah (4/284).

(2) Neno hili linamaanisha muonekano mbaya na mtu kuwa katika hali ya kuvunjika kunakotokana na huzuni. Al-ifswaahu 'an Ma'aani As-swihaah (4/284).

(3) Maana ya neno "Wa'athaais-safar" ni ugumu wa safari. Maana hii inapatikana kwenye kitabu kiitwacho Al-ifswaahu 'an Ma'aani As-swihaah(4/284).



Inapendekezwa kwa msafiri asisafiri peke yake pasina kuwa na mtu wa kufuatana naye;

kwa maneno ya Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

**"Lau wangetambuwa watu yaliyopo kwenye upweke ninavyotambuwa mimi, asingesafiri msafiri wakati wa usiku akiwa peke yake"**

## Wasafiri wanafaa kumchagua moja wao kuwa kiongozi,

ili iwe rahisi zaidi kukusanya jambo lao pamoja, na kuwafanya kukubaliana zaidi, na lenye nguvu zaidi katika kupata malengo yao.

**Amesema Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:**

**« Watakapotoka watu watatu katika safari yoyote, basi wamfanye mmoja wao kuwa kiongozi »**



## Awe na pupa ya kufanya yale ambayo Mwenyezi Mungu amemuwajibishia miongoni mwa ibada, na kujiepusha na yaliyoharamishwa, na ajipambe kwa tabia njema.

na amsaidie mwenye kuhitajia msaada, na atoe elimu kwa mwenye kuitafuta na kuihitajia, na awe mkarimu kwa mali yake, kwa kuitoa katika masilahi yake mwenyewe na katika masilahi ya ndugu zake na kuwatekelezea mahitaji yao.

## Inafaa aongeze matumizi na vinavyohitajika safarini.

kwa kuwa shida inaweza kumtokea na mambo yakaenda , tofauti.



## Inafaa awe katika safari ni mwenye uso wa bashasha, roho safi.

akijitahidi kuingiza furaha kwa anayesafiri pamoja naye, ili awazoee wengine na azoeleke.

**Anafaa kuwa na subira kwa kila kinachomkuta miongoni mwa muamala mgumu wa wenye kusafiri pamoja naye,** na wanapokwenda tofauti na maoni yake, na aamiliane nao kwa namna iliyo nzuri, ili awe ni mwenye kuheshimiwa baina yao na mwenye kupewa taadhima nyoyoni mwao.

## Inapendekezwa kwa wasafiri wanapofika mahala pa kushukia, wakae pamoja.

Kwa maana, baadhi ya Maswahaba wa Mtume - rehema na amani za Mweyezi Mungu ziwe juu yake - walikuwa wanapofika sehemu ya kushukia, wanatawanyika kwenye njia za milimani na mabonde.

**Akasema Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:**

"Hakika kutawanyika kwenu na kwenda kwenye njia hizi za milimani na mabonde kunatokana na Shetani"

Kwa hivyo, baada ya hapo wakawa wanakusanyika pamoja kiasi kwamba ingekunjuliwa nguo juu yao ingewatosheleza wote.



## Inapendekezwa kwa msafiri atakapofika mahala pa kushukia akiwa katika safari yake au akafika sehemu ya kushukia akiwa hayuko safarini, aombe dua iliyothibiti kutoka kwake Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

«Ninajikinga kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia kutokana na shari ya alichokiumba»

Kwani hakika akiyasema maneno hayo, hatodhuriwa na kitu chochote mpaka atakapoondoka mahala pale.

## Inapendekezwa amtukuze Mwenyezi Mungu (kwa kusema: Allahu Akbar) katika sehemu zenye miinuko, na kumtakasa (kwa kusema: subhanallah) anaposhuka kwenye sehemu na mteremko na mabonde. Amesema Jaabir - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

«Tulikuwa tunapopanda miinuko, tunamtukuza Mwenyezi Mungu (kwa kusema: Allahu Akbar), na tunapoteremka, tunamtakasa (kwa kusema: subhanallah)»

Na wala wasipaze sauti zao kwa kuleta Takbira. Amesema Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

**Enyi watu zioneeni huruma nafsi zenu. Kwani nyinyi hamumuombi kiziwi wala aliye mbali. Hakika Yeye yu pamoja nanyi. Hakika Yeye ni Msikivu, aliye karibu!**

## Inapendekezwa kwenda safari wakati wa usiku na haswa mwanzo wa usiku, kwa maneno ya Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

**Shikamaneni na kusafiri wakati wa usiku, kwani hakika ardhi hukunjwa wakati wa usiku.**

## Inapendekezwa kwake azidishe Dua awapo safarini;

kwa maneno ya Mtume - rehema na amani ziwe juu yake:



# Pili: Twahara (usafi) katika safari

## Ni wajibu kwa msafiri

atilie umuhimu usafi wake. Kwa hivyo, atachukuwa udhu kutokana na hadathi ndogo na ataoga kutokana na Janaba.

## Na ikiwa hakupata maji

au ikiwa ana maji machache anayoyahitajia kwa ajili ya kupikia na kunywa, basi atafanya Tayammam.



Aipige ardhi kwa mikono (kwa ndani ya mikono) yake miwili, na aupake uso wake na viganja vyake kwayo.

## Na namna ya kutayammamu ni

## Twahara ya kutayammam ni twahara ya muda tu.

Kwa hivyo, wakati wowote akipata maji, tayammamu yake inaharibika, na itamlazimu kuyatumia maji. Na ikiwa alifanya tayammamu kwa sababu ya kupata

Janaba kisha akapata maji

## basi itamlazimu kuoga;

Na kama akitayammam kwa sababu ya kukidhi haja kubwa kisha akapata maji, basi itamlazimu atawadhe. Imekuja katika hadithi kwamba:

> «Udongo safi ni udhu wa Muislamu hata kama atakosa maji miaka kumi. Akiyapata maji, basi amche Mwenyezi Mungu na ayagusishe kwenye mwili wake»

## Kupangusa juu ya khofu mbili

la kisheria katika Qur'ani na Sunnah na ni makubaliano ya Ahlussunnah.

## Kuna masharti kadhaa kwa ajili ya kupangusa juu ya khofu mbili na chenye kufanana na nazo:

- Khofu mbili hizo au soksi mbili hizi zinapaswa kuwa zinaruhusika na ni safi
- Azifae akiwa na twahara
- Ziwe ni zenye kufunika sehemu za faradhi



**Iwe kupangusa ni katika kupatwa na hadathi ndogo. Hairuhusiki kupangusa kwa kupatwa na Janaba wala kwa jambo ambalo linalazimisha kuoga.**

**Iwe kupangusa ni ndani ya wakati uliowekwa kisheria, nao ni mchana na usiku kwa mkazi, na michana mitatu na masaa yake ya usiku kwa msafiri.**

**Muda huu kulingana na kauli sahihi huanzia pale mtu alipangusa kwa mara ya kwa nza ya baada ya kuharibika kwa udhu, na huisha kwa kutimia masaa 24 kwa mkazi, na kwa masaa 72 kwa msafiri.**



# Na kupangusaji juu ya khofu hubatilika kwa moja kati ya mambo haya matatu:

- Likitokea jambo lenye kuwajibisha kuoga kama vile janaba, basi kunaharibika kupangusa juu ya khofu na inamlazimu mtu huyo kuoga.

- Ikiwa atazivua khofu baada ya kuwa amekwishapangusa juu yake.

- Ikiwa muda unaozingatiwa kisheria utaisha, basi upangusaji utakuwa batili.

* * *



# Tatu: Hukumu za kupunguza swala safarini

## Kupunguza swala katika safari ni bora kuliko kuswali swala kamili

lakini kama msafiri atakamilisha swala rakaa nne, basi swala yake itakuwa ni sahihi lakini atakuwa amekwenda kinyume na kilicho bora.

## Anapunguza swala msafiri atakapokuwa ametoka na kuziwacha kabisa nyumba zote za kijiji chake au mji wake

na huu ndio msimamo wa madhebu ya wengi wa maulamaa.



## Ikiwa atasafiri baada ya kuingia wakati wa swala, **ana haki ya kupunguza swala**

kwa sababu amesafiri kabla ya muda wake kwisha.

## Ama kukusanya

swala kati ya Adhuhuri na Alaasiri **na** kati ya Magharibi na Isha

hilo ni Sunna kwa msafiri anapohitajia kufanya hivyo. Itakapokuwa safari imeshika kasi na imeshaendelea, basi afanye litakalokuwa rahisi kwake kama vile kutanguliza au kuchelewesha.



## Ama ikiwa msafiri hana hitajio la kukusanya, basi asikusanye,

mfano awe ameshuka na kukaa mahala ambapo hataki kuondoka hapo mpaka ifike saa ya swala inayofuata, basi lililo bora kwake ni kutokusanya. Kwa sababu hahitaji kufanya hivyo. Na ndiyo maana Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - hakukusanya alipokuwa ameshuka na kukaa Mina katika Hija ya Kuaga kwa sababu hakuhitaji kufanya hivyo.

## Ama swala za sunnah

ataziswali msafiri kwa namna anavyoziswali mkazi. Kwa hivyo ataswali swala ya Dhuha, Tahajjud, Witiri na zinginezo miongoni mwa swala za sunna isipokuwa sunna za kabla na baada ya swala ya Adhuhuri, Maghari na Isha. Sunnah katika hizo ni kuwacha kuziswali.

## Ni sahihi kuswalia swala za sunnah juu ya kipando:

kama vike ndege, gari, meli na vyombo vinginevyo vya usafiri. Ama swala za Faradhi, hizo ni lazima kuteremka kwa ajili ya kuziswalia chini isipouwa itakaposhindikana.



# Swala ya msafiri anayeswali nyuma ya mkazi ni sahihi

na atakamilisha msafiri kama swala ya imamu , wake. Ni sawa ameikuta swala yote au amekuta rakaa moja au chini ya hivyo. Hata kama ataingia pamoja naye katika Tashahhud ya mwisho kabla ya kutoa salamu, basi atakamilisha swala hiyo bila kufupisha. Hivi ndiyo sahihi kutoka katika kauli za wanazuoni.




# Nne: Adabu za kurudi kutoka katika ibada ya Hija, Umra au safari

**Anapaswa afanye haraka kurudi na wala asikae muda mrefu katika safari pasina kuwa na haja ya kukaa muda mrefu**

kwa maneno ya Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

**(Safari ni kipande cha adhabu. Inamzuia mmoja wenu kula na kunywa na kulala kwake. Kwa hivyo, akimaliza mmoja wenu hitajio lake, basi na afanye haraka arudi kwa watu wake)**

**Na akitaka kurudi kwenye mji wake, atasoma dua ya safari wakati wa kupanda kwake kipando chake**

na atazidisha kwa kusema: **Aaibuuna taaibuuna aabiduuna lirabbina haamiduuna (Tunarejea, tunatubia, tunafanya ibada na tunamsifu Mola wetu Mlezi)**

**Inapendekezwa kwa msafiri wakati wa kurudi kutoka safari yake aseme kilichothibiti kutoka kwa Mtume - rehema na amani ziwe juu yake - alipokuwa akirudi kutoka vitani au Hija au Umra. Alikuwa akipiga takbira katika kila muinuko wa ardhi mara tatu kisha anasema:**

(Laailaha illa llahu wahdahuu laashariikalah, lahul mulku walahul hamdu wahuwa 'alaa kulli shay-in qadiir. Aayibuuna, taaibuuna, saajiduuna, lirabbina haamiduuna. Swadaqallahu waa'dahu, wanaswara 'ab-dahu, wahazamal ahzaaba wah-dahu (Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu mmoja peke yake, asiye na mshirika. Ni wake ufalme na sifa njema ni zake, naye ni Muweza wa kila kitu. Tunarejea, tunabatubia makosa yetu, tu naabudu, tunasujudia na tunamsifu Mola wetu Mlezi. Alitimiza Mwenyezi Mungu ahadi yake, na alimnusuru mja wake, na aliyashinda makundi ya maadui peke yake)



## Inapendekezwa kwa msafiri atakapouona mji wake, aseme hivi:

**Aayibuuna, taaibuuna, 'aabiduuna, lirabbinaa haamiduuna (Tunarudi, tunatubia, tunaabudu, na tunamuabudu Mola wetu Mlezi)**

na ayarudirudie maneno hayo mpaka auingie mji wake. Hii ni kwa sababu Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alifanya hivyo.

## Asije kwa mke wake usiku ikiwa alika mbali kwa muda mrefu pasina kuwa na haja ya kuja usiku isipokuwa ikiwa aliwafikishia kuwa anakuja,

na akawapa habari kwamba atafika usiku. Hii ni kwa sababu Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alikataza hilo. Amesema Jaabir ibnu Abdillah - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

**(Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikataza kwamba mwanamume asiwapigie hodi familia yake usiku)**

Na miongoni mwa hekima ya kutofanya hivyo, ni vile riwaya nyingine ilivyotafsiri:

**(Ili mwanamke mwenye nywele zilizotimka achane nywele zake, na mwanamke ambaye mumewe hayuko anyoe nywele za sehemu za siri)**[4]

---

(4) Neno "Ash-shaa'tha" linamaanisha mwanamke mwenye nywele matimtimu ambazo hazijapakwa mafuta kwa muda mrefu. Na "Al-istihdaad" ni kutumia alaa iliyotengenezwa kwa chuma kama vile wembe katika kunyoa sehemu za siri. Nalo neno "Al- maghiiba" ni mwanamke ambaye mume wake amekaa mbali na yeye kwa muda mrefu. Tazama At-Tahriir fii sharh Swahih Muslim, cha Al-Asbahaaniy (292)

Na katika riwaya nyingine:

**(Alikataza Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - mwanamume kuwagongea watu wa familia yake usiku ili kuchunguza kama wanamfanyia khiyana au kutafuta makosa yao)**

**Inapendekezwa kwa mwenye kutoka safarini aanzie msikiti ambao upo jirani naye na aswali humo rakaa mbili;**

kwa sababu Mtume -rehema na amani ya Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikuwa akifanya hivyo.



## Inapendekezwa kwa msafiri atakapofika kutoka safarini, awaonyeshe huruma watoto wa nyumbani kwake na majirani zake na awafanyie wema watakapompokea.

Imepokelewa kutoka kwa Ibnu Abbas - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kwamba alisema: Alipofika Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, katika mji wa Makkah, walimpokea watoto wadogo wa Banii Abdul Mutwalib. Basi akambeba mtoto mmoja mbele yake na mwingine mgongoni kwake." Naye Abdullahi ibnu Jaafar - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alisema:

**(Alikuwa Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - anaporudi kutoka safarini, analakiwa pamoja nasi. Basi siku moja alilakiwa pamoja nami na Hassan au Hussein na akambeba mmoja wetu mbela yake na mwingine nyuma yake mpaka tunaingia Madinah)**

## Inapendekezwa kutoa zawadi, kwa kuwa kutoa zawadi kuna furahisha nyoyo na kuondoa chuki.

Na inapendekezwa kuikubali zawadi na kulipa juu yake. Na inachukiza kuikataa pasina kuwepo kizuizi cha kisheria. Ndiyo maana amesema Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

**(Peaneni zawadi, mtapendana)**

Na zawadi ni sababu miongoni mwa sababu za kuleta upendo baina ya Waislamu.



## Akifika msafiri katika mji wake, imependekezwa kukumbatiana,

kwa sababu ya yale yaliyothibiti kutoka kwa Maswahaba wa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi mungu ziwe juu yake - kama alivyosema Anas - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

**(Walikuwa wanapokutana, wanasalimiana mikononi, na wanaporudi kutoka safarini, wanakumbatiana)**

# تعرف على الإسلام

## بأكثر من 100 لغة

موسوعة القرآن الكريم
QuranEnc.com

ترجمات متقنة لمعاني القرآن الكريم بأكثر من (75) لغة

بيان الإسلام
byenah.com

مواد منتقاة للتعريف بالإسلام وتعليمه بأكثر من (120) لغة

موسوعة الأحاديث النبوية
HadeethEnc.com

ترجمات متقنة للأحاديث النبوية وشروحها بأكثر من (60) لغة

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

مواد منتقاة للحجـــاج والمعتمرين و الزوار بلغات العالم

جامع المحتوى الإسلامي باللغات
islamcontent.com

مواد إسلامية متنوعة وشاملة بأكثر من (125) لغة

موسوعات وخدمات إسلامية باللغات
s.islamenc.com

للمزيد
من المواقع الإسلامية
بلغـــات العـــالم


ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات